

# **HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA**

## **IDARA YA ARDHI NA MALI ASILI**

### **1.0 UTANGULIZI**

Idara ya Ardhi na Mali Asili inajumuisha vitengo vya Ardhi, Upimaji na ramani, Uthamini, Mipango Miji, Misitu na Nyuki. Vilevile kwa kushirikiana na idara ya ujenzi, idara hii inashughulika na kutoa vibali vya ujenzi.

### **2.0. UTEKELEZAJI WA SHUGHULI MBALIMBALI KATIKA IDARA**

Idara ya Ardhi na maliasili katika Halmashauri ya wilaya ya imeweza kushughulikia na kusimamia masuala mbalimbali yahasuyo sekta ya Ardhi. Masuala hayo ni pamoja na

- i. Kusimamia ukusanyaji wa kodi ya Ardhi (Land Rent).
- ii. Kusimamia shughuli za upimaji wa viwanja vya makazi, biashara na huduma za jamii katika mji wa Nduguti unaofanywa na kampuni binafsi kwa makubaliano rasmi na wananchi.
- iii. Kutoa elimu kwa wananchi katika maeneo mbalimbali yenye migogoro hasa kwenye maeneo yenye wakulima na wafugaji, wakulima wakubwa na wanavijiji na migogoro ya mashamba makubwa.
- iv. Kuendelea kupokea maombi na kutoa hati za umiliki za viwanja na mashamba yaliyopimwa.
- v. Kufanya upimaji wa mashamba ya watu binafsi na taasisi katika vijiji mbalimbali ndani ya wilaya.

### **2.1. MAFANIKIO**

Idara ya Ardhi na maliasili katika Halmashauri ya wilaya ya Mkalama katika kipindi tajwa hapo juu imefanikiwa.

1. Tumepima viwanja 7000 katika mji wa Nduguti ambapo ndio makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama.
2. Kutatua mgogoro wa ardhi baina ya wilaya ya Mkalama na Mbulu, wataalam wa pande zote mbili wamekutana maeneo yenye migogoro ya Hilamoto na Kidarafa kubaini mipaka halali.
3. Kutoa ushauri wa kitaalam na elimu kwa wananchi juu ya masuala yahasuyo Ardhi na Maliasili ofisini na maeneo mbalimbali ndani ya wilaya.
4. Utaratibu wa kutoa Hati miliki unaendelea na fomu za maombi ya miliki zilizopokelewa mpaka tarehe 27/12/2017 ni Thelatini na nane (38).
5. Maombi binafsi ya upimaji yanapokelewa idarani na kufanyiwa taratibu za upimaji.

### **3.0. CHANGAMOTO.**

Idara ya Ardhi na maliasili katika Halmashauri ya wilaya ya Mkalama inakumbana na changamoto zifuatazo;

1. Kutokuwa na Afisa Ardhi Mteule mpaka sasa. Jambo hili linakwamisha juhudi za ofisi za kumilikisha wananchi ardhi ambayo tayari imepimwa kisheria vilevile kuikosesha halmashauri mapato.
2. Kutokuwa na wataalamu wengine katika sekta ya Ardhi na mali asili ikiwemo Mthamini. kuendelea kuazima wataalamu kutoka Manispaa ya Singida hasa kwa kada za Uthamini na Afisa Ardhi Mteule.
3. Kutokuwepo vifaa hasa vya upimaji na uaandaji wa ramani, na kuendelea kukodi vifaa vya upimaji kama differential GPS kwa ajili ya kupima na kutatua migogoro ya mipaka.
4. Tatizo la usafiri jambo linalokwamisha kufanya shughuli za kutosha za nje ya ofisi.

.....

John M. Langas

**KAIMU MKUU WA IDARA YA ARDHI NA MALI ASILI  
HALMASHAURI YA WILAYA MKALAMA**